



**USAID**  
FROM THE AMERICAN PEOPLE



# Kusoma Kiswahili

Kitabu Cha Mwanafunzi Cha I



PHOTO: Christopher Steel

KUSOMA KISWAHILI: KITABU CHA MWANAFUNZI CHA I



PHOTO: SIL

# Kusoma Kiswahili Cha Mwanafunzi

## Yaliyomo

<b>Shukrani</b>	<b>ii</b>	Wiki ya 15	70
Wiki ya 1	1	Wiki ya 16	75
Wiki ya 2	5	Wiki ya 17	80
Wiki ya 3	10	Wiki ya 18	85
Wiki ya 4	15	Wiki ya 19	90
Wiki ya 5	20	Wiki ya 20	95
Wiki ya 6	25		
Wiki ya 7	30	Wiki ya 21	100
Wiki ya 8	35	Wiki ya 22	105
Wiki ya 9	40	Wiki ya 23	110
Wiki ya 10	45	Wiki ya 24	115
		Wiki ya 25	120
		Wiki ya 26	125
Wiki ya 11	50	Wiki ya 27	131
Wiki ya 12	55	Wiki ya 28	136
Wiki ya 13	60	Wiki ya 29	141
Wiki ya 14	65	Wiki ya 30	146

## Shukrani

Kitabu hiki cha wanafunzi kimefanikishwa kutokana na ufadhili wa DFID na USAID/Kenya. Katibu wa Kudumu wa Wizara ya Elimu Profesa George Godia alihusika sana katika kuelekeza juhudi za kitaaluma za Wizara ya Elimu, Baraza la Mitihani nchini Kenya (KNEC), Taasisi ya Wasimamizi wa Elimu ya Kenya (KEMI), Taasisi ya Elimu Maalum ya Kenya (KISE), na Tume ya Kuwaajiri Walimu (TSC). Kwa pamoja, DFID na USAID wanawasilisha kitabu hiki kwa Wizara ya Elimu kwa minajili ya utafiti katika shule zilizo chini mradi wa kuboresha ujuzi wa hisabati na usomaji nchini (PRIMR). **Kitabu hiki ni cha utafiti na matumizi yake nje ya shule zilizo kwenye mradi wa PRIMR hayaruhusiwi.**

Shukrani maalum zawaendea kikundi cha wataalamu kilichoandika kitabu hiki kutokana na mwongozo wa mawanda na mfuatano ulioundwa kwa ushirikiano na Wizara ya Elimu. Shukrani kwa Dkt. Sylvia Linan-Thompson kwa kuongoza uundaji wa mwongozo wa mawanda na mfuatano wa Kiswahili. Shukrani pia kwa kikundi saidizi cha kitaalamu kinachojumuisha Dkt. Agatha van Ginkel, Dkt. Hellen Inyega na Prof. Angelina Kioko. Hongera na shukrani pia kwa kikundi cha kitaalamu cha RTI PRIMR: Dkt. Benjamin Piper, Jody Roy, Titus Kazungu, Sarah Koko, Isaac Cherotich, Samuel Ogwang, Salome Ong'ele na Jessica Mejia kwa bidii yao katika kuandika kitabu hiki.

Shukrani maalumu ni kwa kikundi cha Uanzilishi na Utekelezi wa Mradi (PDIT) kinachojumuisha washiriki wa Wizara ya elimu na Wadau wengine. Kikundi hiki kiliongoza ruwaza ya mpango huu, uanzilishi wa mpangilio wa mawanda na mfuatano. Pia kiliandika mipangilio ya masomo na kinasimamia majaribio ya nyenzo hizo madarasani. Kikundi kingine kinajumuisha Washauri wa walimu (TAC Tutors), makocha, walimu katika shule za PRIMR kikundi cha kwanza. Mchango wao katika kuboresha nyenzo hizi unatambulika sana. Pia wanafunzi na washiriki wa jamii katika kaunti ya Nairobi, Kiambu, Nakuru na Kisumu walihusika kwa kiwango kikubwa. Ubora wa kazi hii unatokana na juhudi zao za dhati.

Shukrani pia kwa Masudi Ramadhan Abdi na Apollo Erik kwa uchoraji wa picha. Hatimaye ni bidii, uwezo na talanta ya wanafunzi wa nchi ya Kenya ambao watupa motisha kuendeleza na kufanikisha mradi huu.

Mei 2013

★	m	M
👁️	anaona	paka mama

Koki na Mugambi



Siku ya 3

★	a m
👄	m a ma a a
👁️	na
🗣️	ma ma mama a ma ama

Siku ya 4

★	A M
👄	m a ma a a
🗣️	ma ma mama a ma ama



**Mama na Paka**

Mama anaona paka.

Paka anaona mama.





Siku ya 5

★	m M      a A						
☪	m a      ma      a      a						
👁️	mama      paka      anaona      na						
🗣️	mama      ama						
🏠	<table border="1"> <tr> <td>ma</td> <td>a</td> <td>mama</td> </tr> <tr> <td>a</td> <td>ma</td> <td>ama</td> </tr> </table>	ma	a	mama	a	ma	ama
ma	a	mama					
a	ma	ama					





Katumbo




Siku ya 1

	u	m	a
	m u u	mu u	m a a ma a
	ma ma ma u a	mama maua	u a u ma ua uma
		uma	ua

Siku ya 2

	U	M	A
	m a m u	ma mu	u u
	u ma u a	uma ua	a mu a u amu au
	1. aum	2. kapa	3. umaa














## Paka na Ua

Mama anaona uma na maua.  
Paka anaona ua.  
Paka, uma ua!

Siku ya 3

	k m a u
	k a ka k aa kaa k u ku k uu kuu
	ku ku kuku ka ka kaka u ku ta ukuta a mu a amua
	1. kaka 2. kuku

Siku ya 4





	K M A U
	k a ka m a ma k u ku m u mu
	ku kaa kukaa u kuu ukuu ma kaa makaa ma kuu makuu
	a ka amua akaamua a ka uma akauma a ka mu uma akamuuma
	1. ukuk 2. kaak 3. amam



### Paka na Kaka


Paka akaamua kukaa.  
Mama akaamua kukaa.  
Kaka akaamua kukaa.  
Kaka akamuuma paka.  
Paka akamuuma kaka.

## Siku ya 5






★	u k	U K
	k u ku k a ka	m a ma k aa kaa
	kuu kuu ka ka ma ta tu	kuukuu kaka matatu
	a ka amua a ka uma	akaamua akauma
	ma ka u ka kaa mu k a	makaa ama

## Mama na paka






Paka na mama.  
Mama anaona paka au ua?  
Mama anaona paka.  
Paka anaona mama au ua?  
Paka anaona mama.



## Siku ya 1

	t	u	k
	t a ta t aa taa		t u tu k a ka
	ta ka taka	ka ta kata	a mu amu
	takataka	amu	kata kaa
	1. kaa		2. kata

## Siku ya 2

	T	U	K
	t a ta t aa taa		m a ma k u ku
	ta ka taka u kuu ukuu		ku kaa kukaa ma kaa makaa
	taka taka ku mu uma ku mu ua		takataka kumuuma kumuua
	1. atak	2. akatakat	3. aak



## Kaka na Amu






Kaka anaona takataka.

Mama anaona takataka na kata. Amu anaona takataka,  
kata na kaa.






Kaa ataka kumuuma amu.

Amu akataka kumuua kaa.

## Siku ya 3

	i	t	k
	t i ti i i	m i t ii	mi tii
	ki ti i ta	kiti ita	ki ma u ki
	kata		
	1. kima	2. mkuu	

## Siku ya 4

	I	K	U
	t i ti t ii	ti tii	t a ta t u tu
	ti ki ti ka taa	tikiti kataa	m kuu i nu a
	a ka kaa a ka kataa	akakaa akakataa	a ka taka a ka ona
	1. kuum	2. itikit	3. maki



### Mama, Amu na Kima Mkuu

Mama akaona Kima mkuu.

Kima mkuu akaona mama.

Mama ana tikiti na uki mtamu.

Kima mkuu akataka kukaa na mama na amu.

Amu akakataa kukaa na kima mkuu na mama.

Mama akakataa kukaa na Amu. Mama akakaa na kima mkuu.




## Siku ya 5

★	i t	I T
☺	t a ta t u tu	k i ki t ii tii
🗣️	ka ta kata ki ma kima	i nua inua ki ti kiti
📖	mama <b>an</b> akaa mama <b>an</b> ataka	mama <b>at</b> akaa mama <b>at</b> ataka
🏠	ma mi mu ta ka ki ku tu	tatu kiti





## Amu na Kaa

Amu ataka matatu kuukuu na taa.






Kaa ataka takataka na makaa. Kama amu atataka takataka na makaa, kaa atakataa katakata.



## Siku ya 1

	n	t	i
	n a n i	na ni	n u nu
	a na ta i	ana tai	ka ki m ti ni kaki mtini
	1. kaki		2. tai

## Siku ya 2





	n	t	i
	n a na	k a ka	m a ma
	m ti ni a na kaa	mtini anakaa	m kuu mkuu
	a na a na a na a na	ona taka tamani kataa	anaona anataka anatamani anakataa
	1. ait	2. timni	3. ikka








## Tai Mkuu


Tai mkuu anakaa na paka mtini. Paka ana kaki. Tai mkuu anaona paka na kaki. Tai mkuu anataka kaki. Paka anakataa. Tai mkuu anathamani kumuua paka. Paka anakataa kukaa na tai mkuu mtini. Tai mkuu ana.....

Siku ya 3

	o n
	n o no k o ko o o m o mo t o to
	no no nono mo to moto mo to ni motoni m to to mtoto ko no ko no konokono
	1. mtoto 2. moto

Siku ya 4

	O N
	n o no n a na n u nu n i ni
	m to ni mtoni m ku ki mkuki ku u a kuua ku o ta kuota
	kono kono konokono a na toka anatoka a na kataa anakataa i na nukia inanukia
	1. tomtoto 2. kokonono 3. tomoni



### Kanini na Katana


Kanini ni mtoto. Anakaa na kaka Katana. Katana anaona Kanini akikata kuni na kuota moto. Motoni kuna ini nono. Katana anatoka mtoni na mkuki. Katana anaona konokono. Anatoa mkuki na kuua konokono. Katana anataka kuoka konokono motoni. Kanini anakataa.

## Siku ya 5





★	n N	o O												
👄	n o no n a na	t o to n i ni												
🗣️	mo to moto m ka te mkate	no no nono m ti ni mtini												
📖	mkate <b>u</b> nanukia mti <b>u</b> nanukia	mikate <b>i</b> nanukia miti <b>i</b> nanukia												
🏠	<table border="1"> <tbody> <tr> <td>m</td> <td>to</td> <td>mo</td> <td>i</td> <td>kaa</td> <td>ni</td> </tr> <tr> <td>a</td> <td>na</td> <td>ta</td> <td>ka</td> <td>u</td> <td>no</td> </tr> </tbody> </table>	m	to	mo	i	kaa	ni	a	na	ta	ka	u	no	moto
m	to	mo	i	kaa	ni									
a	na	ta	ka	u	no									

## Kamau na Tikiti






Kamau ananunua tikiti, kaimati, uki, na maini. Koki anatamani kaimati na uki. Kamau anakataa. Koki anataka maini. Kamau anakataa. Koki anatamani tikiti. Kamau anamkatia tikiti. Tikiti ni tamu.



Siku ya 1

	w	n	o
	w a wa	w i wi	
	w u wu	w o wo	
	wa tu watu	wa na wana	
	wa to to watoto	wa ta no watano	
	1. watoto	2. watatu	

Siku ya 2

	W	N	O
	w a wa	k o ko	
	n a na	w o wo	
	wa ta no watano	wa tu watu	
	wa to to watoto	wa na wana	
	m ta ma mtama	m ta mu mtamu	
	wa ka taka	wakataka	
	a ka wa ona	akawaona	
	wa ka wa toa	wakawatoa	
	1. totowa	2. twaano	3. tutami







## Watoto wa kima






Kima ana watoto watano. Kila mtoto wa kima ana mikia mitatu. Watoto wakataka mtama mtamu wa mama. Mama akawaona watoto wa kima mtamani. Mama akawaita watu. Watu wakawatoa watoto wa kima mtamani. Unataka kuwaona watoto wa kima wa mikia mitatu?



## Siku ya 3

	e	w
	n e ne w e we	t e te m w e mwe
	te na tena m ke ka ni mkekani	nee ma neema ma we mawe
	1. mwewe	2. mawe

## Siku ya 4

	E	e	
	w e we w i wi	k o ko m w e mwe	
	mwe we mwewe mo to moto	m ka te mkate m ti ni mtini	
	a ka mwona a ka mwita a ka m timua a ka m kamata	akamwona akamwita akamtimua akamkamata	
	1. mewwe	2. mwae	3. mteka



### Neema na Mwewe

Amina akaketi mkekani akiota moto. Akamwona mwewe akimkamata kuku. Akamwita Neema. “Neema, Neema?” Neema akaitika. “Ee, Amina.” Amina akaita tena. “Neema! Ona mwewe.” Neema akatoka na mawe akamtimua mwewe. Mwewe akatua mtini. Amina na Neema wakaketi mkekani wakiota moto na kukata mkate.

## Siku ya 5

★	w W	e E												
☺	t e te w a wa	w i wi k e ke												
🗣️	wa tu wo te wa to to	watu wote watoto												
📖	Wewe unataka Wewe unaona	Mtoto anataka Mtoto anaona												
🏠	<table border="1"> <tr> <td>wa</td><td>tu</td><td>m</td><td>ka</td><td>te</td><td>mi</td> </tr> <tr> <td>i</td><td>a</td><td>to</td><td>ma</td><td>we</td><td>ta</td> </tr> </table>	wa	tu	m	ka	te	mi	i	a	to	ma	we	ta	watu
wa	tu	m	ka	te	mi									
i	a	to	ma	we	ta									





## Tai na Mtoto wa Paka

Owino ana watoto watatu:  
Wata, Wakio na Waki.  
Watoto wa Owino wana  
mtoto wa paka. Tai mtini  
anamuona mtoto wa paka.









Anatamani kumkamata mtoto wa paka. Watoto  
wanaita. Owino anamuona tai na mtoto wa paka. Owino  
anaokota mti. Kwa nini Owino anaokota mti?

## Siku ya 1

	l w e
	l e le l i li l a la l u lu l o lo
	lo la ni lolani ka li kali ki ti ni kitini li ma u limau
	1. Lolani 2. limau

## Siku ya 2





	L l
	l a la l e le w i wi l o lo k e ke
	Ne li ma Nelima u ki uki le te a letea m ka te mkate
	a ka m letea akamletea a ka litema akalitema li li kuwa lilikuwa
	1. mauli 2. alik 3. wamu 4. tikini








### Lolani na Nelima

Lolani alilala kitini. Nelima akamletea limau. Lolani akala. Lo! Limau lilikuwa kali. Lolani akalitema limau na kulia. Nelima akaona Lolani akilitema limau. Nelima akamletea Lolani muwa. Lakini Lolani hakula muwa. Nelima akamletea uki. Lolani akala uki. Uki ni mtamu.

## Siku ya 3

	h w e i
	h a ha h o ho h u hu h e he h i hi
	ha lu a halua ha mu hamu ka ha wa kahawa ho te li hoteli
	1. halua 2. iliki

## Siku ya 4





	H h
	h a ha k a ka l a la w o wo h o ho
	ka ma kama la ki ni lakini ho te li hoteli
	<b>alinunua hakununua</b> <b>alitokea hakutokea</b> <b>aliletea hakuletea</b> <b>alitaka hakutaka</b>
	1. luaha 2. ikili 3. hakawa 4. liwa



## Hotelini


Helena alinunua halua, iliki na kahawa hotelini. Alikuwa na hamu ya kahawa tamu. Mama akatokea na kuketi kitini. Helena akamletea kahawa tamu na halua. Lakini mama alitaka kula wali kwa maini. Hakutaka kahawa tamu na halua kama Helena.

## Siku ya 5

★	I L	h H												
	l e le h a ha	h u hu h o ho l u lu k a ka												
	lu lu li ma u	lulu limau ho te li ta u lo												
	<b>Umoja</b> akamletea mtoto akamwona mtoto	<b>Wingi</b> wakawaletoa watoto wakawaona watoto												
	<table border="1"> <tbody> <tr> <td>te</td> <td>ta</td> <td>ho</td> <td>te</td> <td>li</td> <td>na</td> </tr> <tr> <td>la</td> <td>we</td> <td>ma</td> <td>ti</td> <td>ni</td> <td>le</td> </tr> </tbody> </table>		te	ta	ho	te	li	na	la	we	ma	ti	ni	le
te	ta	ho	te	li	na									
la	we	ma	ti	ni	le									





## Ali na Lina

Ali aliokota lulu. Akaiweka katika taalo. Lina akaiona taalo kitini. Akaitoa taalo na kuiweka uani. Akaona lulu na kuiokota. Ali akamuona Lina na lulu. Ali akataka lulu. Lina akakataa. Ali akalia na kuita mama. Lina akaiweka lulu kitini. Ali akaitwaa ile lulu.










Siku ya 1

	s	l	h
	s a sa s o so		s i si s e se
	sa na sana su ku ma sukuma		u si ku usiku sa ma ki samaki
	1. tausi		2. sikio

Siku ya 2





	S	L
	s a sa l a la	h a ha s u su
	si ki o sikio ku m tu si kumtusi	na na si nanasi ki su kisu
	wasi wasi su ku ma wiki a ka sononeka a li m tesa	wasiwasi sukumawiki akasononeka alimtesa
	1. usita 3. nasina	2. masaki 4. siwasu








## Mateso ya Tausi

Tausi alikaa Kisii na Amu. Kila siku Amu alimtesa na kumtusi sana. Siku moja Amu alimuuma Tausi sikio. Siku moja, Amu alimtuma usiku kununua sukumawiki, samaki na nanasi. Usiku huo, Tausi alisononeka na kuwa na wasiwasi sana. Wasusi wakamwona. Wakaamua kukaa na Tausi.

Siku ya 3

	b	s
	b a ba b u bu	b e be b o bo
	ba ba baba a su bu hi asubuhi	bi si bisi ba ku li bakuli
	1. bisi	2. bakuli

Siku ya 4





	B	b
	b a ba b u bu b o bo	b e be k a ka m k a mka
	m ke be bu i bu i	mkebe a m ka amka bu i bu i buibu
	Wa li amka Wa ka tamani wa ka toa Wa ka tabasamu	wali amka waka tamani wakatoa wakatabasamu
	1. sibi	2. kuliba
	3. lauribi	4. ibuibu



## Bisi

Asubuhi baba, mama na watoto waliamka. Watoto wakatamani kula bisi. Kulikuwa na bakuli, bilauri na mkebe kabatini. Mama akatoa bakuli akaona bibo. Watoto wakatoa bilauri wakaona buibui. Baba, akamtoa buibui. Watoto wakatoa mkebe. Wakaona bisi. Wakatabasamu.

## Siku ya 5





★	s S	b B
	b a ba m k a mka	b u bu w e we
	ba ba baba	m ke be mkebe
	<b>Umoja</b> Mtu <b>akamw</b> ona kuku Mtu <b>akamk</b> amata kuku	<b>Wingi</b> Watu <b>wakawa</b> ona kuku Watu <b>wakawa</b> kamata kuku
	si ku u sa ba ki ma li na bu i ha	

## Wasia wa Babu






Babu aliwaita watoto wote na kusema, “Sikieni wasia huu. Nawasihi msome. Masomo ni muhimu. Masomo huleta hekima. Hekima huleta mali.” Watoto wakasema, “Naam Babu. Sisi sote tutasoma. Usiwe na wasiwasi.” Babu akasema tena, “Msisahau kuwasiliana na walimu wenu.”



Siku ya 1

	y	s	b
	y a ya y i yi		y e ye y u yu
	ma ya i u ki wa	mayai ukiwa	a su bu hi ye ye yeye
	1. yaya		2. mayai

Siku ya 2





	Y	L
	y o yo l a la	y a ya b l a bla
	ha yu ko ka bla	hayuko kabila
	hu tu simamia ku ya elewa a na ye tii a ta ku somea	hutusimamia kuyaelewa anayetii atakusomea
	1. ayya 3. kayahe	2. yaima 4. yeey







## Yaya wetu

Yaya wetu ni Halima. Kila asubuhi wakati mama hayuko, yeye hutuokea keki na mayai. Kabla ya kulala, yeye hutusimamia kuyaelewa masomo yetu. Ukiwa mtoto anayetii, Halima atakusomea hekaya wakati wa kulala. Tunampenda Halima sana.

## Siku ya 3

	z s b y
	z a za z i zi z u zu z e ze
	zi zi zizi za bi bu zabibu zi wa ni ziwani za mu zamu
	1. zamu 2. zizi

## Siku ya 4

	Z z
	z o zo s a sa z i zi s i si
	na zi nazi tu zo tuzo wa za zi wazazi mi za bi bu mizabibu
	wa li kuwa walikuwa ku tazama kutazama wa li elekea walielekea ku wa bebea kuwabebea
	1. muza 2. iziz 3. zimina 4. wanizi





## Zani na Ziki

Wakati wa likizo Zani na Ziki walikuwa na zamu ya kutazama zizi lao. Kila asubuhi walielekea ziwani. Huko waliona minazi na mizabibu. Walikula zabibu na kubebea wazazi wao nazi. Wazazi wakawatuza: Zani tuzo la zeze, na Ziki tuzo la miwani.

## Siku ya 5





★	y Y	z Z
👄	y a ya z o zo	y e ye z u zu
🗣️	za bi bu wa za zi	zabibu wazazi
📖	hu tu simamia hu tu ambia	hutusimamia hutuambia
🏠	si ka ya wa za na l ha zi ma ki ti	

## Yatima Ayoo






Ayoo ni yatima. Yeye hukaa na babu wake wilayani Kikuyu. Ayoo na babu wake hawana mali. Ayoo anatamani mayai. Kila siku Ayoo husali ili babu wake awe na mali. Kwa sasa yeye hula sima kwa mabuyu. Mabuyu yamo kibuyuni.



## Siku ya 1

	g	y	z
	g a ga g e ge		g aa gaa g i gi
	ki so go ma ge go ma go ti gaa gaa		kisogo magego magoti gaagaa
	1. mizigo		2. mtego

## Siku ya 2

	G	g
	g u gu m z o mzo	z o zo g o go
	m te go mtego mi guu miguu	m zo zo mzozo mu u gu zi muuguzi
	wa ka watega wa ka gaagaa ha wa kuweza i li o watuliza	wakawatega wakagaagaa hawakuweza iliowatuliza
	1. zigomi 3. guumi	2. temgo 4. sokigo








### Wezi Sokoni

Katika soko la Mogotio, kulitokea wezi wa mizigo sokoni. Watu wakawatega. Mtego ukawakamata. Wakataka kukimbia. Wakaumia. Kuna walioumia kisogo, magego, magoti, na miguu. Wezi wakagaagaa. Muuguzi akawatibu. Akawasugua kwa miti iliyowatuliza. Wakasamehewa. Kutoka siku hiyo wezi hawakuweza kuiba tena.

Siku ya 3

	d y z g
	d e de d i di d u du d o do d a da
	de be debe do li doli o di di odidi da ki ka dakika
	1. daga 2. dania

Siku ya 4

	D z
	d a da b a ba d e de b e be b u bu
	da ni a dania ba a da baada go do ro godoro go lo li gololi
	a li ita aliita wa ka elekea wakaelekea tu ta nunua tutanunua ku ni nunulia kuninunulia
	1. gaada 2. niada 3. bede 4. logoli



### Odidi na Baba Sokoni

Baba aliita, “Odidi! Amka! Leo ni siku ya soko.” Odidi aliamka baada ya dakika kidogo. Wakaelekea soko la Gede. Baba akasema, “Odidi, leo tutanunua daga, dania, debe na godoro.” Odidi akauliza, “Baba, unaweza kuninunulia soda, doli na gololi?” “Naam Odidi.” Baba akaitikia.

## Siku ya 5





★	g G d D
☺	g i gi g e ge d i di
🗣️	go do ro godoro go lo li gololi
📖	alisema hakusema aliteta hakuteta
🏠	m te go de be ki da ma ka ti ge mu

## Kazi ya Kogo na Odhis






Kogo na Odhis walikaa Migori. Kazi yao ilikuwa kubeba mizigo mizito. Kila asubuhi walibeba magunia mazito ya maboga na mihogo. Kila usiku mabega na miguu yao iliama sana kutokana na kazi yao. Walikula ugali kwa uyoga, na kugawana hela baada ya kazi.



## Siku ya 1

	j	g	d
	j a ja	j a a jaa	
	j e je	j i ji	
		ji tu jitu	
		ji we jiwe	
		Ji lo Jilo	
	Ju ma ta no	Jumatano	
	1. jitu	2. kijijini	

## Siku ya 2

	J	j	
	j o jo	j u ju	n e ne n ne nne
	I ju maa	Ijumaa	
	Ju ma nne	Jumanne	
	ki ji ji ni	kijijini	
	ma ja ni ni	majanini	
	ha wa kwamini	hawakwamini	
	wa ka mwamini	wakamwamini	
	wa na kijiji	wanakijiji	
	1. tuji	2. weji	3. maajui 4. jijikini














## Jilo na Jitu

Siku ya Jumatatu, Jilo aliona jitu. Akasema, “Nimeliona jitu majanini.” Wanakijiji hawakwamini. Siku ya Jumanne, Jumatano na Alhamisi akaliona jitu tena. Siku ya Ijumaa Jitu likasema, “Jilo, nataka kula.” Jilo alijawa na wasiwasi. Akalipatia jitu jiwe la moto. Jitu likala lile jiwe na kuzimia. Wanakijiji wakamwamini Jilo.

## Siku ya 3

	r g d j
	r e re r a ra r i ri r o ro
	ga ri gari ra di radi ja nu a ri januari m ka e mkae
	1. Januari 2. Rais

## Siku ya 4





	R r
	r u ru j u ju w e we m w e mwe
	mwe zi mwezi Ra i s Rais zi a ra ziara ma du ka ni madukani
	bara bara barabara a ki maliza akimaliza wa ka torokea wakatorokea
	1. isra 2. iara 3. razia 4. rabaraba



## Ziara ya Rais


Mwezi wa Januari, Rais wetu alikuja kijijini kukutana na raia. Gari lake lilisimama barabarani. Rais akasema, “Nawasihi mkae kwa amani na watu wote.” Siku hiyo, wanakijiji walikuwa na raha sana. Akimalizia ziara yake, mara tukasikia radi. Watu wakatorokea madukani. Barabara ilijaa maji.

## Siku ya 5

★	j J	r R
	r a ra r e re	j i ji r a ra r o ro l a la
	Ju ma nne I ju maa mwe zi	Jumanne Ijumaa mwezi
	wanakata mkate wanataka mtama	hawakati mkate hawataki mtama
	kaa ma mu ka a maa ku m kuu ma	mama amka makaa

## Jino la Zakayo

Jumamosi asubuhi, Zakayo alilala kitini. Jino lake lilikuwa linamuuma. Alijilaza huku akilisugua jino kwa kidole. Mara akajikokota kuelekea jikoni.



Huko aliokota jivu na kuliweka jinoni. Mama yake alimuona ameketi jikoni akilia. Alielekea dukani akanunua dawa akamletea. Zakayo alimeza dawa. Jino lake likatulia.

Siku ya 1

★	m a u k																		
☺	m a ma k a ka m u mu k u ku m aa maa m uu muu k aa kaa k uu kuu																		
🗣️	ka ka kaka ku u kuu ma kaa makaa ma ma mama u ma uma a m ka amka																		
📖	<b>aka</b> amua kuamka <b>waka</b> amua kuamka <b>aka</b> muuma kaa <b>waka</b> muuma kaa																		
🏠	<table border="0"> <tr> <td>kaa</td><td>ma</td><td>mu</td><td>ka</td><td>a</td><td>mama</td> </tr> <tr> <td>maa</td><td>ku</td><td>m</td><td>kuu</td><td>ma</td><td>amka</td> </tr> <tr> <td></td><td></td><td></td><td></td><td></td><td>makaa</td> </tr> </table>	kaa	ma	mu	ka	a	mama	maa	ku	m	kuu	ma	amka						makaa
kaa	ma	mu	ka	a	mama														
maa	ku	m	kuu	ma	amka														
					makaa														

Paka na Kaa

Kuku akaamua kuamka.  
 Paka akaamua kuamka.  
 Mama akaamua kuamka.  
 Kaka akaamua kuamka.  
 Kaka akaamua kukaa na kaa.  
 Kaa akamuuma kaka. Paka  
 akamuuma kaa.



Siku ya 2





★	tT	iI	nN	oO		
👄	t a ta n i ni	t i ti n a na	t o to t u tu			
🗣️	m ti ni i ni	mtini ini	mi mi ni na	mimi nina		
📖	Kono a ka	kono itika	Konokono akaitika			
🏠	ni	m	na	ta	mi	tamu
	mu	ti	i	nu	ma	mimi

Tai na kima

Tai anakaa mtini na konokono. Kima akaona tai na konokono. Kima akaita, “Tai, nataka kununua konokono.” Tai akaitika, “Konokono ananuka. Mimi nina ini nono.” Kima akaitika “Kama konokono ananuka nitanunua ini nono.” Kima akaoka ini nono. Ini nono ni tamu.



Siku ya 3

★	wW	eE	lL	hH		
	w e l e	we le		wi wi li li		
	mi aka mi wi li	miaka miwili		wa tu watu la ki ni lakini		
	a li m ku wa	hukumu tukana		alimhukumu kuwatukana		
	ka	mi	wi	li	wa	miwili
	ki	a	tu	ha	wi	hawa

**Katana ahukumiwa**

Halima ni hakimu katika mahakama kuu. Alimhukumu Katana kwa kulewa na kuwatukana watu. Katana alihukumiwa miaka miwili. Katana alilia. Akamaka, "Miaka miwili! Ee Mola, Niokoe." Wakili wa Katana alilalamika. Lakini hakimu alikuwa amenena.




Siku ya 4

★	sS	bB	yY	zZ
👄	s a sa y a ya	s o so z i zi	s aa saa z o zo	
🗣️	wa ya waya mo to moto	ma yo we ma ha li mahali		
📖	wasi wasi tu li sikia		wasiwasi tulisikia	
🏠	wa mo sti sa mi bi to ya ba ma		saba waya	





Waya wawaka moto

Tulisikia mayowe tukiwa sebuleni! “Tokeni!” Baba akasema. Sote tukatoka na kutazama. Tukaona moto ukiwaka kwa kasi. Waya wa stima uliwaka moto. Sote tukawa na wasiwasi. Wazima moto wakatokea. Wakauzima moto uliokuwa umewaka. Mioyo yetu ikatulia, tukaelekea tena sebuleni.





Siku ya 5





★	g G	d D	j J	r R
	j a ja g o go	j e je d i di	j i ji b i bi	
	Ja nu a ri Fe bru a ri Ju la i	Januari Februari Julai		
	wa ka kasirika wa ka ripoti	wakakasirika wakaripoti		
	ni ju ma se mba go a sti de mbe	Juni		

Miezi






Januari na Februari kuna joto na jua kali. Watoto wanasoma sana. Baada ya likizo wao husoma Mei, Juni hadi Julai. Agosti kuna likizo tena. Watoto hufurahi kusaidia wazazi. Wao hurudi kusoma miezi mitatu hadi likizo ya sikukuu ya Desemba.



Siku ya 1

	p
	<p>p a pa p e pe p i pi</p> <p>p u pu p o po w a wa</p> <p>p w a pwa</p>
	<p>pa sa ka pasaka pa te pate</p> <p>pu nda punda pa pa papa</p>
	<p>pasaka pate</p>

Siku ya 2





	P
	<p>p e pe b e be</p> <p>w e we p w e pwe</p>
	<p>Pe te ro Petero</p> <p>pi a pia</p> <p>M pe ke to ni Mpeketoni</p> <p>pwe za pweza</p>
	<p>wa li safiri walisafiri</p> <p>wa li tumia walitumia</p> <p>wa li po fika walipofika</p>
	<p>tepa sapaka zapwe apap</p>







## Sikukuu ya Pasaka

Sikukuu ya pasaka iliwadia. Petero na wazazi wake walitoka Pate na kuelekea Lamu. Walitumia gari lao hadi Mpeketoni. Hapo walipanda dau na kuvuka Bahari ya Hindi hadi kisiwani Lamu. Kule kisiwani, waliona watu wakitumia punda kwa usafiri wao. Pia waliona samaki aina ya papa na pweza.

Siku ya 3

	f	
	f i    fi    f e    fe    f o    fo f a    fa    f u    fu	
	fa na ka    fanaka fu ra hi    furahi fa gi a    fagia fo le ni    foleni	
	darasa	walifagia

Siku ya 4

	f	
	f e    fe    k e    ke    s k e    ske w a    wa    k w a    kwa	
	fa ra si    farasi m ti ha ni    mtihani ba i s ke li    baiskeli kwa o    kwao	
	radasa    lefoni rasafa    nakafa	



## Matokeo ya Pili

Pili alifaulu katika mthani wa darasa la nane. Kijiji kizima kilifurahi sana. Wanakijiji walifagia barabara ikawa safi. Walifurahi na kupiga vigelegele. Walisafiri kwa kutumia farasi, basi, matatu na hata baiskeli. Wakapiga foleni ili wamsalimie Pili. Wazazi wake walifurahi sana kwa fanaka ya mtoto wao.

## Siku ya 5





★	p P	f F
☺	p e pe f e fe b a ba	p i pi p a pa p o po
🗣️	m sa fi ri mwa li mu e ro p le ni	msafiri mwalimu eroplени
📖	watu <b>walifika</b> watu <b>walienda</b>	watu <b>walipofika</b> watu <b>walipoenda</b>
🏠	ni pa fa ra ha fi ba si na ka sa ri	pasaka

## Usafiri

Kila mtu hutamani kusafiri kwa njia za kifahari. Njia hizi ni kama eroplени, magari na meli. Ukiwa unaenda safari fupi, ni bora kusafiri kwa miguu. Kusafiri kwa miguu kuna faida kwa binadamu. Zaidi ya hayo, msafiri hatumii pesa zozote kusafiria.



Siku ya 1

	v	p	f
	v e v u	ve vu	v i v a vi va
	vi ji to vi ja na	vijito vijana	vi li ma vi bo ko vilima viboko
		vijito	vilima

Siku ya 2

	v		
	f o f e	fo fe	v e v o ve vo
	vi ji to ni vi si ma	vijitoni visima	ma de vu ma devu ku pa nda kupanda
	ya li malizika vi ka haribiwa I ta bidi	yalimalizika vikaharibiwa Itabidi	
		vitoji tavio	limavi simavi







## Ukataji wa miti






Kijijini Lodwa kulikuwa na vijito na vilima. Vijana wa huko walikuwa wavuvi wa samaki. Kwa sababu ya watu kukata miti, maji yalimalizika vijitoni. Viboko na samaki wakafa. Viota vikaharibiwa. Mzee Madevu akawaita watu na kusema, “Tunahitaji kupanda miti ili tupate maji kwa visima.”



## Siku ya 3

	sh			
	sh o sh i	sho shi	sh e sh a	she sha
	shu le ni di ri sha ni ma je shi ku wa sha	shuleni dirishani majeshi kuwasha		
	shuleni		dirisha	

## Siku ya 4

	Sh			
	sh i sh u	shi shu	s i s u	si su
	ni sha ni ma shu jaa m ko ro sho ki sha	nishani mashujaa mkorosho kisha		
	a li huzunika wa ka ji tayarisha wa ka shikana	alihuzunika wakajitayarisha wakashikana		
	nileshu	dishari	dasha	shaki



## Aisha na Shiko

Aisha alifika shuleni mapema kukutana na rafiki yake Shiko. Akasimama dirishani na kutazama wanajeshi wakijitayarisha kwa siku ya mashujaa. Mara Shiko akatokea. Wakashikana mikono kwa furaha. Kisha wakaamua kufagia karibu na mkorosho. Baadaye waliwasha moto majani na takataka. Siku hiyo walipewa nishani na shada la maua na mwalimu mkuu.

Siku ya 5

★	vV	fF	Sh				
👄	v a sh a	va sha	v u f e vu fe sh o v e sho ve				
🗣️	ki sha ma shu jaa		kisha mashujaa				
📖	<b>dereva alifurahi</b> <b>tumbili alifurahi</b>		<b>madereva walifurahi</b> <b>tumbili walifurahi</b>				
🏠	di	vi	bo	ko	sha	ma	viboko
	ri	ji	to	li	le	shi	





Dereva Mvivu

Kulikuwa na dereva aliyekuwa mvivu sana. Siku moja akasimamisha gari lake barabarani. Akala viazi vitamu na kulala huku akijifunika kwa vazi lake.









Vikosi vya tumbili vikamvamia. Tumbili wakasukuma gari na kulipeleka msituni. Wanyama msituni wakaogopa na kutoroka. Gari likaharibika. Ndipo dereva akaamka na kushangaa kilichotendeka. Tumbili walifurahi sana huku wakishangilia.

## Siku ya 1

	ny	v	sh
	ny a ny e	nya nye	ny i ny u nyi nyu
	nyu ki Nya ma ri wa nya ma nye sha		nyuki nyamari wanyama nyesha
	nyikani		nyara

## Siku ya 2




	Ny		
	ny a n e	nya ne	n a ny e na nye
	nya ra nyi ka ni ku nye sha nyo ro ro		nyara nyikani kunyesh nyororo
	ku ka nyesh wa li po kuwa wa ka m tafuta wa ka toroka		kukanyesh walipokuwa wakamtafuta wakatoroka
	kanyini	ranya	ronyoro inyuk








## Nyamari Nyikani

Siku moja, Nyamari alikuwa nyikani. Usiku huo, kukanyesha sana. Akasikia wanyama wakilia nyikani. Jamii yake wakamtafuta kote. Watu wabaya wakaja na kumteka nyara. Walipokuwa wakikaza mikono na miguu yake kwa nyororo, nyuki wakaja na kuwauma wale watu. Hao, wakatoroka. Nyamari akawa huru. Naye hakuenda nyikani tena.

## Siku ya 3

	dh	
	dh a dha dh i dhi	dh e dhe dh o dho
	fe dha dha ha bu bi dha a	fedha dhahabu bidhaa
	ndani	bidhaa

## Siku ya 4





	Dh	
	dh a dha dh i dhi	d a da d i di
	Ko dhe k to fa u ti da ni a	Kodhek tofauti dhania
	kina meta meta a li po fika a ka m pasua	kinametameta alipofika akampasua
	aabidh	feadh niada ninda



## Kodhek Atajirika


Kodhek alitaka kununua bidhaa tofauti tofauti. Siku hiyo hakuwa na fedha za kutosha. Jioni moja, akanunua samaki mdogo na dania. Alipofika kwake, aliweka samaki mezani, kisha akampasua. Kodhek akapata kijiwe kidogo ndani ya samaki. Akakiosha kijiwe na akaona kinametameta. Alipojua ni dhahabu alifurahi sana. Kodhek akaiuza dhahabu hiyo. Akatajirika.

## Siku ya 5

★	ny	Ny	dh	Dh			
	dh o dh i	dho dhi	ny e ny u	nye nyu			
	nya ra nyi ka ni nyo ro ro		nyara nyikani nyororo				
		<b>alipojua</b> <b>alipofika</b>	<b>walipojua</b> <b>walipofika</b>				
	<b>nyu</b>	<b>nya</b>	<b>ki</b>	<b>ra</b>	<b>nyo</b>	<b>dha</b>	wali
	<b>ma</b>	<b>ri</b>	<b>wa</b>	<b>ro</b>	<b>re</b>	<b>u</b>	





## Usafi

Watoto wa Shinyanya hawakuwa wasafi. Hawakuoga wala kusugua meno. Nyayo zao zilipasuka hata zikawa na vidonda. Miili yao pia iliparara. Kwao hakukuwa kusafi. Nyuki, nyigu, panya na nyoka waliamia huko. Watoto wale waliila nyama bila kuipika vizuri. Wakapata minyoo. Wakaugua. Nyanya yao aliwapa dawa na kuwashauri wawe wasafi.










Siku ya 1

	th			
	th a	tha	th u	thu
	th i	thi	th e	the
	the la	thi ni	thelathini	
	the ma	ni ni	themanini	
	nyati		nyoka	

Siku ya 2





	Th			
	th a	tha	t a	ta
	t o	to	th o	tho
	dha ti		dhati	
	nya ti		nyati	
	the la	thi ni	thelathini	
	a li po	thibitisha	alipothibitisha	
	ha ja	thubutu	hajathubutu	
	a me	mu ibia	amemuibia	
	tidha	tinya	mathani	kanyo








## Nyati na Nyoka


Nyati na Nyoka walikuwa marafiki wa dhati. Walikaa pamoja hata wakati wa jua kali. Nyoka alikuwa na miaka themanini. Nyati alikuwa na miaka thelathini. Nyoka alikuwa na vitu vya thamani. Siku moja nyati akamuibia. Nyoka akajua kuwa Nyati amemuibia. Urafiki ukaisha. Tangu siku hiyo Nyati hajathubutu kukaa karibu na Nyoka tena.

Siku ya 3

	ch			
	ch a	cha	ch i	chi
	ch o	cho	ch e	che
	chu i	chui	chu ra	chura
	m che zo	mchezo		
	chatu		chura	

Siku ya 4

	ch			
	ch u	chu	j u	ju
	h u	hu	ch o	cho
	chu pa	chupa	wa li che za	walicheza
	ki cho cho ro	kichocho		
	a li hesabu	alihesabu	a ka hesabu	akahesabu
	ku hesabu	kuhesabu		
	uchat	urach	chemzo	pachu



### Mchezo wa Chatu, Chura na Chui


Chatu, Chura na Chui waliishi kwenye Kichocho. Siku moja walicheza mchezo wa kuhesabu nyota. Chatu alihesabu na kupata nyota kumi tu. Chui naye alihesabu hadi ishirini. Chura alihesabu kutoka thelathini, arobaini, hamsini, sitini, sabini, themanini, tisini hadi mia moja. Chui alikasirika sana. Akamweka Chura kwenye chupa.

## Siku ya 5





★	th	Th	ch	Ch
👄	ch a ch i th o	cha chi tho	j a h i h o	ja hi ho
🗣️	chu ra chu pa		chura chupa	
📖	chui alikasirika chui alimweka		chui atakasirika chui atamweka	
🏠	the lu ji cha ra che ma ni tha i che ki			theluji

## Nyororo za thamani

Tabitha alikuwa na nyororo kumi za dhahabu. Kijana mmoja akasema, “Ukinipatia hizi nyororo kumi, nitazifanya ziwe thelathini.” Tabitha akasema, “hata kama utazifanya ziwe themanini, sikupi.” Tabitha alijua thamani ya nyororo hizo. Kutoka siku hiyo, hakuthubutu kuziweka hadharani tena.



Siku ya 1

	gh	th	ch
	gh e gh u	ghe ghu	gh o gh a
	gho ro fa gha li gha si a	ghorofa ghali ghasia	
	viatu	ghasia	

Siku ya 2





	Gh		
	gh a h a	gha ha	g a k a
	ki ji ji ni su ru a li sha ti ma shi mo	kijijini suruali shati mashimo	
	tu ka shangaa ya ka raruka wa ka mu umiza vi li onekana	tukashangaa yakararuka wakamuumiza vilionekana	
	siagha	ofiak	ligha tuvia








### Adhabu ya Mwizi

Kulitokea ghasia kijijini kwetu. Mimi na wazazi wangu tuliishi ghorofa ya tatu. Mara tukashangaa kuona mtu akipigwa. Watu wakamuumiza. Mavazi yake yakararuka. Suruali na shati lake zikawa na mashimo. Kofia na viatu vyake vilionekana kuwa ghali sana. Baadaye jirani akasema alikuwa ameiba vitu sokoni.


Siku ya 3

	ng	th	ch	gh
	ng e	nge	ng u	ngu
	ng o	ngo	ng a	nga
	ra ngi		rangi	
	shi ngo ni		shingoni	
	ma ko nge		makonge	
	sha nga		shanga	
		ngozi	shanga	

Siku ya 4

		Ng	ng	
	ng a	nga	g a	ga
				m a ma
	we ngi	ne	wengine	
	ru ngu		rungu	
	ngo zi		ngozi	
	ma va zi		mavazi	
	ya me	badilika	yamebadilika	
	ha wa	ku vaa	hawakuvaa	
	ku fukuzia		kufukuzia	
	vi li	kuwa	vilikuwa	
	zingo	ngasha	ngira	guruu





### Mavazi ya kale

Zamani za kale babu na bibi zetu hawakuvaa mavazi ya bei ghali. Walivaa nguo za ngozi kiunoni. Pia walivaa shanga za rangi mbalimbali shingoni. Viatu vyao vilikuwa vya miti, ngozi na makonge. Wengine walibeba rungu ili kujikinga na kufukuza wanyama wa msituni. Siku hizi mambo yamebadilika. Watu wanavaa watakavyo. Mavazi hayana heshima wala kujali utamaduni wetu.

## Siku ya 5





★	ng	Ng	gh	Gh			
👄	ng i	ngi	ng a	nga			
	gh a	gha	gh i	ghi			
🗣️	ru ngu		rungu				
	we ngi ne		wengine				
📖	nilikuwa		sikuwa				
	nilicheza		sikucheza				
🏠	gha	sha	li	o	ngo	ra	ngozi
	nga	ru	ngu	zi	ngi	ndi	

## Mavazi ya Mama Fatuma






Fatuma alikuwa chumbani. Mvua ikaanza kunyesha kwa ghafla. Kukawa na gharika. Mama alikuwa ghalani akitoa nafaka. Mavazi yake yalikuwa uani. Nikakimbia na kutoa buibui, rinda, gauni, sketi, kamisi, na blauzi ya mama. Kwa kawaida mavazi ya mama huwa ghali sana. Na yeye huwa hapendi kupata gharama zaidi.




Siku ya 1

	ng'	gh	ng
	ng' a ng' u	ng'a ng'u	ng' i ng' o
	ng'o mbe ng'a mbo ng'a ng'a	ng'ombe ng'ambo ng'ang'a	
	ng'ambo	ng'ara	

Siku ya 2





	Ng'		
	ng' a ng e	ng'a nge	ng a ng' e
	ng'a mbo a ka ng'o a za ku ng'a ra	ng'ambo akang'oa zakung'ara	
	a li hudhuria za ku ng'a ra a ka ng'oa	alihudhuria zakung'ara akang'oa	
	mbong'a	peunye	mbeng'o naki



### Ng'ang'a auza Ng'ombe


Ng'ang'a aliishi peke yake ng'ambo ya mto. Siku moja, alitaka kuhudhuria maonyesho ya kilimo sokoni. Siku hiyo, alivaa nguo nyeupe za kung'ara. Alipofika mtoni, akang'oa mti ili apime kina cha maji. Alipofika ng'ambo ya mto, Ng'ang'a aliuza ng'ombe wake. Kisha akanunua bidhaa mbalimbali. Alirudi akiwa na furaha sana.

## Siku ya 3

	ia	oa	ea	ua
	u	u	e	e
	a	a	o	o
	to a	toa	o te a	otea
	tu a	tua	ti a	tia
	mvivu		uongo	

## Siku ya 4

	-ua	-ea	-ia
	w a	wa	y a
	w o	wo	y u
	zo e a	zoea	
	zo a	zoa	
	si ki a	sikia	
	a me	zoea	amezoea
	a ka	puuza	akapuuz
	a ka m	zuia	akamzuia
	vivum	ongou	kuoaz
			amuazi



## Kima Mvivu

Kima alizoea kuwa mvivu. Msimamizi wake akasema, “Acha uvivu.” Kima hakutii. Msimamizi akamzuia kuzoa takataka siku hiyo. Kima akasema uongo ili apewe kazi yake tena. Msimamizi akasema atulie na kungoja uamuzi wa kamati kuu. Kima akapuuza maagizo. Akafutwa kazi.

Siku ya 5





★	ng'	Ng'												
☺	ng i    ngi	ng a    nga												
	ng' a    ng'a	ng' u    ng'u												
🗣️	ng'o mbe	ng'ombe												
	ng'a mbo	ng'ambo												
📖	leo <b>amezoea</b>													
	jana <b>alizioea</b>													
	kesho <b>atazoea</b>													
🏠	<table border="1" style="display: inline-table; text-align: center;"> <tr> <td>ng'o</td> <td>mbe</td> <td>ng'a</td> <td>ki</td> <td>ma</td> <td>ri</td> </tr> <tr> <td>mbo</td> <td>a</td> <td>si</td> <td>sa</td> <td>fa</td> <td>ng'e</td> </tr> </table>	ng'o	mbe	ng'a	ki	ma	ri	mbo	a	si	sa	fa	ng'e	sikia
ng'o	mbe	ng'a	ki	ma	ri									
mbo	a	si	sa	fa	ng'e									

Amu safarini





Amu alifunga safari. Akaenda kwa Oenga. Yeye na Oenga wakala mayai ya kukaanga. Walipomaliza, walielekea eneo la wazi kulikokuwa na ua la maua. Walitoa mkeka na kuulalia. Waliwaona kuku waliokuwa wameangua vifaranga. Mwewe alipowakaribia, walimtimua.




Siku ya 1

	-ao	-io
	a o ao	i o io
	u ba o ubao la o lao ki fa gi o kifagio mbi o mbio	ki fu ti o kifutio kwa o kwao si o sio
	wao	ubaoni

Siku ya 2

	-uo	-ia	-eo
	ki fu ti o shi ka moo da ra sa ni ki cho nge o	kifutio shikamoo darasani kichonge o	
	a ki ingia hu mu amkua ku andika mwa limu m kuu	akiingia humuamkua kuandika mwalimu mkuu	
	uboa	fukitio	owa aonibu













## Darasa la Maria


Maria yuko darasa la kwanza. Mwalimu wake anaitwa Bi. Nerea. Bi. Nerea akiingia darasani, wanafunzi humuamkua “shikamoo”. Darasa lao ni kubwa. Kwenye kuta kuna saa na chati. Darasa lina ubao mweusi. Mwalimu wao hutumia chaki kuandika ubaoni. Kila mwanafunzi huwa na kitabu, kalamu, kifutio na pia kichonge.

Siku ya 3

	u	a	e	o	i
	b a	ba	d a	da	
	p a	pa	b o	bo	
	Ki o ko		Kioko		
	wa na tu li a		wanatulia		
	ta bi a		tabia		
		nzuri	kioko		

Siku ya 4

	u	a	e	o	i
	ku m be be a		kumbebea		
	ali ku wa		alikuwa		
	pi a		pia		
	wa na tulia		wanatulia		
	a li hakikisha		alihakikisha		
	wa li furahishwa		walifurahishwa		
	wa li po chagua		walipochagua		
	nzakwa	rinzu	biata	nikwai	



### Kiranja Wetu Kioko


Kioko alikuwa kiranja wa darasa la kwanza. Alihakikisha wanafunzi wanatulia darasani. Alikusanya na kumbebea mwalimu vitabu. Kabla ya mwalimu kuingia darasani, Kioko alihakikisha ubao umefutwa. Mwalimu alifurahishwa na kazi ya Kioko. Wanafunzi pia walimpenda kwani alikuwa na tabia nzuri. Kila walipochagua kiranja, Kioko alichaguliwa.

## Siku ya 5





★	u U	a A	e E	o O	i I	
👄	i a e a	ia ea	o o u a	oo ua	i o io	
🗣️	mwe u si		mweusi			
	ki fu ti o		kifutio			
📖	<b>alichagua</b>		<b>hakuchagua</b>			
	<b>alifuta</b>		<b>hakufuta</b>			
🏠	u	ba	o	li	mu	pia
	pi	u	mwa	ta	bi	ubao

## Somo la Wanyama






Ijumaa iliyopita, wanafunzi wa darasa la kwanza walisoma kuhusu wanyama. Mwalimu alitumia chati ya wanyama kufunzia somo hilo. Kwenye chati kulichorwa ngamia, kondoo, ng'ombe, mbuzi na jimbi au jogoo. Wanafunzi waliimba wimbo kuhusu wanyama tofauti. Baadaye mwalimu aliwaletea redio. Wakasikiza somo la redio. Wanafunzi walifurahia sana.




Siku ya 1

	m			
	m t o	mto	s a	sa
	m s a	msa	b e	be
	m b e	mbe	p a	pa
	m p a	mpa	m e	me
	m m e	mme	g o	go
	m me a	mmea	m go mba	mgomba
	m to	mto	mbe gu	mbegu
	mambo		fimbo	

Siku ya 2





	m			
	m f a	mfa	m s a	msa
	m p a	mpa	m t a	mta
	m w a	mwa	m b a	mba
	ka je	mbe	kajembe	
	cha	mbo	chambo	
	mba	a zi	mbaazi	
	fi	mbo	fimbo	
	mbali		karibu	
	funga		fungua	
	nyingi		chache	
	mbama	mbocha	gomimba	mbofi








## Kajembe

Kajembe aliishi karibu na mto. Mto ulikuwa na mamba lakini Kajembe hakuogopa kuvua samaki. Alitumia fimbo na chambo. Pia alilima kutumia jembe lake. Alikuwa na migomba na miembe. Pia alikuwa na mbegu za mbaazi na mboga. Mara nyingi alijifunga kilemba, huku akiimba na firimbi yake.

Siku ya 3

	n	
	n d a nda n z a nza	n j a nja n ch i nchi
